




**SHIRIKA LA UMEME  
TANZANIA**

**MEGAWATI  
2115  
UMEME  
ZINAKUJA**

**BWAWA LA  
KUFUA UMEME LA  
MWALIMU JULIUS NYERERE**

**JUNI, 2022**



Mradi wa Bwawa la Kufua umeme la Julius Nyerere (**JULIUS NYERERE HYDRO POWER PROJECT**) ulianza **15 Disemba 2018** baada ya kusainiwa mkataba. Kazi rasmi za ujenzi zilianza **14 Juni 2019**, na mpaka sasa kazi inaendelea.

Serikali kupitia TANESCO inaendelea na utekelezaji wa mradi huu mkubwa na wa kimkakati wa kufua umeme kwa maji wa bwawa la Julius Nyerere utakaozalisha **Megawati 2115** za umeme.


Upatikanaji wa umeme wa Julius Nyerere ni sawa na ongezeko la **asilimia 136** zaidi ya uwezo wa sasa wa **megwati 1,694.55** kwenye gridi ya Taifa. Mradi huu wa **bwawa la Julius Nyerere ni mkubwa Afrika mashariki na wa 4** kwa ukubwa **barani Afrika**.

Kukamilika kwa mradi huu mkubwa kutapelekea kuwa na umeme wa gharama nafuu, uhakika na vilevile kuchangia katika pato la Taifa. Mradi wa Julius Nyerere - JNHPP umeajiri wafanyakazi zaidi ya **11060**, **asilimia 90** ikiwa ni watanzania na **asilimia 10** wakiwa ni wageni.

# UJENZI WA MRADI HUU UNA SEHEMU KUU NANE



## 1. TUTA KUU (MAIN DAM)

  
**69.24%**

Tuta Kuu yaani (Main Dam) la kuhifadhi maji ya bwawa la Julius Nyerere imefikia **asilimia 69.24**, Tuta linajengwa kwa sehemu tatu yani upande wa kushoto, kulia na kati. Tuta lote lina jumla ya urefu wa mita 1025 na kimo cha mita 190 kutoka usawa wa bahari. Kukamilika kwa ujenzi wa tuta hili na miundombinu wezeshi kutapelekea kuanza kwa zoezi la kujaza maji kwenye Bwawa la Nyerere.

## 2. MAHANDAKI YA KUPITISHA MAJI

(POWER WATER WAYS)



80.72%

Mahandaki ya kupitisha maji ni eneo lingine ambalo lipo katika utekelezaji wa mradi ni njia kuu tatu za mahandaki ya kupitishia maji ya kuendeshea mitambo, (Power Water ways). Utekelezaji wa eneo hili umefikia **asilimia 80.72**.

Mahandaki haya matatu, ndipo ambapo maji kutoka kwenye bwawa yatakapopita kwenda kwenye mashine 9 za kuzalisha umeme. Eneo hili inaenda sambamba na ujenzi wa **matanki matatu** (Surge Tanks), ambapo mpaka sasa matanki haya ambayo ni kwa ajili ya upumuaji wa mahandaki wakati wa uzalishaji umeme yameshakamilika kwa kiasi kikubwa.





### 3. JENGO LA MITAMBO

(POWER HOUSES)



47.85%

Power House ni jengo la mitambo, ambapo hapa itasimikwa mitambo 9 yenye uwezo wa kufua umeme wa megawati 235 kila mmoja. Kazi za ujenzi pamoja na usimikaji wa mitambo zinaendelea. Na limefikia **asilimia 47.85**.



### 4. KITUO CHA KUSAFIRISHA UMEME

(SWITCH YARD)




84.74%

Kituo cha kusafirisha umeme ni kituo cha kupokea na kusafirisha umeme wa Kilovoti 400 kutoka kwenye mashine umba (transformer) 27 zilizopo kwenye jengo la mitambo (Power House). Eneo hilo umeme unaozalishwa na mitambo ya JNHPP utapokelewa na kusafirishwa kupitia njia mbili za msongo wa kilovoti 400 kuelekea Chalinze na kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa. Ujenzi katika eneo hili upo katika hatua nzuri, kwani tayari umekwisha kamilika kwa **asilimia 84.74**.


## 5. KINGO ZA KUZUIA MAJI (SADDLE DAM)



  
47.47%

Bwawa la Nyerere, lina kingo nne za kuzuia maji (Saddle Dams), zenye urefu wa **kilometa 17.4**, ambapo kazi ya kingo hizo ni kuzuia maji yasitoroke kwenye maeneo ya bwawa yenye mabonde hivyo kuhifadhi maji kwa ajili ya uzalishaji wa umeme. Utekelezaji wake umefikia asilimia **47.47**.

## 6. DARAJA LA KUDUMU (PERMANENT BRIDGE)



  
94.5%

Utekelezaji wa ujenzi wa Bwawa la Nyerere unaenda sambamba na ujenzi wa miundombinu ya kudumu ikiwemo **daraja kubwa na la kisasa** litakalo rahisisha usafirishaji wa vifaa vyote vya ujenzikwenda kwenye mradi lakini pia ndio daraja litakalotumika **kuunganisha mikoa ya kusini na pwani** kupitia kijiji cha Nyamwage kata ya muhoro Rufiji. Daraja hili linauweza wa kubeba hadi tani 250 za mizigo na ujenzi umefikia asilimia **94.5**.

## 7. NYUMBA ZA KUDUMU

(PERMANENT HOUSES)



71.01%

Ujenzi wa Makazi ya Kudumu kwa ajili ya wafanyakazi wa mradi wa Bwawa la Nyerere umefikia asilimia **71.01**. Nyumba nyingi zimekamilika na nyingine zinaendele kukamilika.


## 8. BARABARA ZA KUDUMU

(PERMANENT ROADS)

Ujenzi wa barabara za kudumu zenye urefu wa kilomita 26 za kiwango cha lami unaendelea. Barabara hizi zitayaunganisha meneo yote yenye miundombinu ya kudumu na pia baadhi yake zitatumika kama sehemu ya barabara kuu ya kuunganisha mkoa wa **Pwani na mikoa ya Kusini** kupitia **Nyamwage kata ya muhoro Rufiji**. Kazi katika eneo hili zinaendelea.



## MAMBO MUHIMU KUTAMBUA



01

Umeme unaozalishwa Julius Nyerere unaingizwa kwenye gridi ya Taifa ili kuwafikia watumiaji, tayari ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya kilovoti 400 na kituo cha kupoza umeme cha Chalinze (Chalinze substation) umeshaanza, hadi sasa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme umefikia **asilimia 48**.

Utekelezaji wa mradi wa Julius Nyerere umeambatana na **faida za kimazingira** zitakazo saidia kupunguza athari za mafuriko kwa wananchi wanaoishi kwenye vijiji vya **mto rufiji kutokana na bwawa kuhifadhi maji**.

02

03

• Ikumbukwe kuwa vijiji hivyo vimekuwa vikikumbwa na mafuriko makubwa kipindi cha mvua kuanzia **miaka ya 1974** kutokana na mto rufiji kupokea maji mengi kutoka vyanzo vya **mto Ruegu, Kilombero na Ruaha Mkuu**





## MWISHO

Serikali ya Awamu ya sita imedhamiria kukamilisha mradi huu katika ubora na kuhakikisha ndoto ya Taifa inatimia, Hadi sasa tayari Serikali imemlipa mkandarasi takribani Trilioni 3.9 kwa wakati ambayo ni sawa na asilimia 60 ya malipo yote ya kimkatiba, na gharama ya mradi hadi kukamilika itakuwa ni Trilioni 6.55.



SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)  
MAKAO MAKUU, KITALU NA. 114,  
BARABARA YA DAR ES SALAAM,  
SLP 453 DODOMA- TANZANIA

**0748 550 000**

 [Tanesco\\_Official\\_Page](#)  [TanescoYetuTz](#)  [TanescoYetuTz](#)

**BWAWA LA KUFUA UMEME LA MWALIMU JULIUS NYERERE**